**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU—TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU**

**SHULE YA SEKONDARI MWANDOYA**

**S.L.P. 160**

**MEATU – SIMIYU**
**Tarehe……………………**

NAMBA ZA SIMU
0754065972/0783259293 – MKUU WA SHULE
0693039529– MAKAMU MKUU WA SHULE

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………**
**S. L. P ……………………………………………**
**……..**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA……. KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWANDOYA HALMASHAURI YA MEATU MKOA SIMIYU MWAKA WA MASOMO…………………………**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha …. katika Shule hii mwaka wa masomo……….na atasoma tahasusi ya **HGL,HGLi** Shule ya Sekondari Mwandoya. Shule inapatikana upande wa kaskazini mwa makao makuu ya wilaya ya Meatu. Muhula wa kwanza wa masomo utanaanza kwa tarehe itakayotangazwa na Mhe. Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.
2. **Usafiri**
   Ukiwa Shinyanga panda gari: Shinyanga - Mwandoya nauli Tsh. 10,000/= Ukiwa Mwanza panda gari: Mwanza - Mwandoya nauli Tsh. 10,000/=
   Ukiwa Bariadi panda gari: Bariadi - Mwandoya nauli Tsh. 5,000/=
   Ukiwa Meatu (Mwanhuzi) panda gari: Mwanhuzi - Mwandoya nauli Tsh. 5,000/=

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Suruali 2 rangi nyeusi kwa ajili ya darasani

ii. Suruali 2 rangi ya damu ya mzee kwa ajili ya kazi za nje (shamba dress)

iii. Mashati 2 meupe mikono mirefu (tetron)

iv. Viatu vya shule vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili Nyeusi

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta rangi ya kijani

viii. Tai mbili rangi Nyeusi

ix. T-shirt rangi nyekundu zenye kola nyeupe mbili

x. T-shirt rangi ya kijivu zenye kola mbili

xi. Sare za michezo raba jozi 1, Tracksuit 1, bukta I na T-shirt 2 rangi ya bluu

xii. Picha nne za wazazi au ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**Tanibihi:**

Mwanafunzi harusiwi kuja na nguo za nyumbani. Unatakiwa kuja na nguo zilizoelekezwa Rangi ya kitambaa imeambatanishwa kwenye fomu hii.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: •

i. Madaftari Caunta book Q4 (8) na Dictionary

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika *(orodha iambatishwe);*

iv. Scientific Calculator;

v. Godoro 1 , size inchi 21/2

vi. Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 Nguo za ndani za kutosha, mto na taulo

vii. Vyombo vya chakula (sahan, bakuli, kijiko na kikombe vya udongo)

viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

ix. Kwanja 1 **(HGL),** jembe lenye mpini **(HGL,HGLi)** 1, reki 1**(HGLi),** mifagio 2 wa ndani **(HGLi),** na nje **(HGL),** na tochi inayotumia betri au mwanga wa jua kwa matumizi ya dharura.

### 2.3 Michango mbalimbali ya shule ilipwe kwenye akaunti ya shule Na.30901100009 NMB SHULE YA SEKONDARI MWANDOYA

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Tafadhali andika jina la Mwanafunzi kwenye PAY IN SLIP YA BENKI na alete PAY IN SLIP kwa Mhasibu wa shule. Hakuna fedha itakayopokelewa mkononi.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)**

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule …..........................................**

**Jina la Mkuu wa Shule: Donald Ndege Maduhu**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**



NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule: 0783259293 / 0754065972
- Makamu Mkuu wa Shule: 0693039529
- Mwandamizi Taaluma: 0787728415
- Mwandamizi Malezi: 0693929291

# FOMU YA KUANDIKISHWA NA AHADI ZA UTII

**(Ijazwe kwa herufi kubwa na irudishwe kwa mkuu wa shule**

1. (a) Jina kamili …………………………………………...
   (b) Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………
   (c) Kijiji/Kata………………… Wilaya…………………….
   Mkoa…………………………
   Taifa…………………………………..
   (d) Dini.................................................
   (e) Shule unayotoka . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .
2. Jina kamili la Baba au Mlezi..........................................Anwani yake……………………
   Kazi ya Baba au Mlezi............................................................
3. **Ahadi za Mwanafunzi**

Mimi………………………………………………………nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule. Nayakubali na niko tayari kuwa mwanafunzi wa Mwandoya sekondari.

Naahidi kwamba

i. Nitatimiza masharti yote ya shule
ii. Nitatii sheria za shule nikikiuka ahadi zangu nitachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

**Tarehe** ………………………………..    **Sahihi ya Mwanafunzi**.............................

**Ahadi za Mzazi**

Mimi.......................................................................................(Mzazi au Mlezi) wa Mwanafunzi..........................................................................................Nimeelewa maelekezo ya shule kwa Mwanafunzi huyu. Hivyo naahidi kwamba;

i. Nitashirikiana kikamilifu na uongozi mzima wa shule katika kumwelimisha na kumlea ipasavyo.
ii. Nitatimiza masharti yake ya shule
iii. Sitamkatiza masomo kwa minajiri ya shughuli za familia kumuoza au mambo kama hayo yanaweza kumfanya aache shule.
iv. Nitafanya kila jitihada kumwezesha mwanangu kuwahi shule kila siku na kufika shuleni siku ya kufungua shule bila kuchelewa.

**Tarehe**………………………    **Sahihi ya Mzazi/Mlezi**..............……………

# MWANDOYA SECONDARY SCHOOL

## MEDICAL REPORT FORM FOR STUDENTS

**PART ONE STUDENT'S PERSONAL DETAILS**

Student names .

**Age** .

Sex .

**PART TWO: MEDICAL REPORT**

1. Tuberculosis .
2. Asthma .
3. Rheumatic fever .
4. Allergic disorder .
5. Heart disease .
6. Dysentery .
7. Viscose veins .
8. Kidney disease .
9. Diabetes .
10. Epilepsy .
11. Deformity .
12. Mental illness .
13. Eye disorder .
14. Ear, nose or throat disorder .
15. Skin disease .
16. Anemia .
17. Gynecological disorder .

**PART THREE: CONCLUSION**

I have personally examined Mr/Miss And consider he/she Is physical and mentally fit/not fit to be admitted to the school for studies.

Name .

Tittle .

Qualification .

Signature .

Official stamp .

Date .

## ORODHA YA VITABU

1. History
    1. Advanced Lerner's History 5/6 Oxford
    2. Mastering History Carter. — Carter.
    3. History for Advanced level. — Zist Kamili
    4. History for Advanced level. — Comrade Shibitali
    5. History for Advanced level. — TIE
2. Historia ya tanzania na maadili
    1. historia ya tanzania na maadili kidato cha tano -- sita TIE

2. Geography.
    1. Physical Geography. — Zist Kamili
    2. Physical Geography. — Bummer
    3. Physical Geography. — TIE
    4. Human Economic. — TIE

3. English language.
    1. Advanced language. — Oxford
    2. English language. — Nicholas Ashel
    3. English language for Advanced TIE

4. English Literature.
    1. Rwanda Magere
    2 His Excellence the head of states
        1. Betray in City

5 Academic communication
    i. Academic communication skills for advanced level - TIE